

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



07 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA – TAREHE 07 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

377. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea TARURA fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kuzingatia ukuaji wa kasi wa Miji na Halmashauri zetu.

378. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Wazazi wanachangishwa michango ya kuchangia Elimu wakati Serikali inasema Elimu kwa Shule ya Msingi na Sekondari ni bure.

379. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kubadili Shule za Msingi za Tarafa ya Ngorongoro kuwa za Bweni ili kunusuru maisha ya Wanafunzi ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu na kuhatarisha maisha yao kutokana na Wanyamapori kwani eneo kubwa la Tarafa hiyo ni sehemu ya Hifadhi.

380. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa mipaka kati ya Vijiji vya Mwanholo na Nyenze dhidi ya Mwekezaji na Mchimbaji Madini Eli Hilal Wilayani Kishapu.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

381. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Wananchi wa Kijiji cha Kintanula Kata ya Mwamagembe katika Jimbo la Manyoni Magharibi mawasiliano ya uhakika ya simu.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

382. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini kinazuia kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya Makutano – Sanzate kwa kiwango cha lami ambayo ina miaka tisa sasa.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

383. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Mambwenkoswe ili kuwapunguzia Wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta haki.

WIZARA YA MAJI:

384. MHESHIMIWA JUMANNE ABDALLAH SAGINI (BUTIAMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Kata za Bwiregi, Nyamimange, Buswahili na Sirorisimba zinapata maji ya Ziwa Victoria kwa kuwa Mradi wa Maji wa Mgango – Kyabakali – Butiama hautazifikia.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

385. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini upanuzi wa Kiwanda cha Sukari cha Ilovo utakamilika na kwa kiasi gani upanuzi huo utaenda sambamba na kuondoa kero ya Mizani na Vipimo vya *Sucrose* kwa Wakulima wa Miwa.



WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

386. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-


Je, ni lini Serikali itakuja na Mpango madhubuti wa kuitumia Bahari kwa Programu za Uvuvi wa Bahari Kuu na michezo ya Bahari

ili kutengeneza ajira kwa Vijana wa Jimbo la Kawe hasa ikizingatiwa nusu ya Jimbo hilo lipo Mwambao wa Bahari ya Hindi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



DODOMA
07 JUNI, 2021

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE